

Shairi la "Masanduku" liliandikwa na Bi Farida Maulid wa Mombasa, Kenya, linazungumzia udanganyifu wa uchaguzi katika nchi ambayo inajitapa kuwa mtari wa mbele kwa demokrasia duniani. Shairi hili pia linataja jina la Mhusika wa uchafu huo herufi ya kwanza katika kila beti inayoambatana na shairi hilo. Mbali ya ubatili wa uchaguzi shairi hili linaendelea kuzungumzia matumizi mabaya ya madaraka, na utawala wa kimabavu ambao, umepuuzwa vyombo vyote vya kimataifa vilivyoanzishwa katika kuepusha vita. Maudhui ni Demokrasia potofu, na utawala wa kibabe ambao haustahili kuwepo kwenye karne hii ya ishirini na moja, ambayo inashuhudia demokrasia pandikizi.

MASANDUKU

1. **G**olegole linatoka, kalamu ni kazi yake,
Gogoteza kusimika, ukweli mahala pake,
Goigoi ameshika, hatamu si haki yake,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
2. **E**bo kura kaziiba, usukani kuushika,
Engaenga imeziba, sera hazikusimika,
Endesha kwa kusiriba, vita kuziunganisha
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
3. **O**ngopa kwa kila jambo, Iraki na uchaguzi,
Okoteza huna tumbo, taaluma huiwezi,
Otama bila kikumbo, hatuhitaji wakwezi,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
4. **R**ui kashika hatamu, amani kuivuruga,
Rukaruka na rujumu, duniani kutuvuga,
Rumande ujihukumu, bila ya kutuvuruga,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
5. **G**obori lafuka moshi, kila kona linafika,
Gubu limekuwa choshi, gubiko lahitajika,
Gugu kama halitoshi, shambani kujipachika,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
6. **E**puka na ufisadi, tayari ulionao,
Elevuka kama jadi, ambayo usiyonayo,
Enzi heshima na taji, kwa watu ulionao,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
7. **W**ahenga walibaini, nasaa kuitifaki,
Wadhiha waliyakini, Wahedi kuwashitaki,
Wahshi na Walakini, wadhifa ulihamaki,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
8. **B**aramaki ni mbumbumbu, ujemadari kapata,
Batuka kama mbumbu, risasi kila akipita,
Bazazi huyu si nyumbu, bali ni mjinga pita,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
9. **U**zuzu unatibika, kwa busara na hekima,
Uzushi siyo uzuka, ukweli utajitwika,
Ubahalulu husika, amani unaizika,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
10. **S**habaki chungu kauli, amani tunahitaji,
Shakiza haistahili, vita kila kitongoji,
Shaghalabaghala ili, kumpumbaza shemeji,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.
11. **H**ashakum si matusi, Kalamu naweka chini,
Hasama siyo harusi, harubu ifichwe ndani,
Hatiani hashu nasi, hati siifichi ndani,
Masanduku kayaficha, na taji kajipachika.

Farida Maulid
Mombasa, Kenya
28th July 2003
